

ASb  
approved



# Ndogo Sana, Kubwa Sana

Brigid Simiyu

Sandy Lightly

Kiswahili





Nelima aliita, "Mama! Njoo uone. Nguo hizi zote ni ndogo kwangu!"

"Hebu nizione," Mama alisema.



"Tangalie hii sketi yangu. Ni ndogo mno," Nelima alisema.

"Ni kweli," Mama alikubali. "Lakini, Sela anaweza kuitumia sketi yako."



"Tazama suruali yangu. Ni ndogo sana," Nelima alisema.

"Kweli, suruali hii ni ndogo sana." Mama alijibu. "Sela anaweza kuitumia suruali yako pia."



"Mama, angalia fulana yangu. Ni ndogo sana," Nelima alisema.

"Ni kweli," Mama alikubaliana naye. "Sela anaweza kuichukuwa fulana yako."



"Angalia sweta yangu. Ni ndogo sana," Nelima alisema.

"Ndiyo, ni ndogo," Mama alijibu. "Sela anaweza kuichukuwa sweta yako."



"Angalia koti langu la mvua. Ni dogo sana," Nelima alisema.

"Kweli, ni dogo," Mama alisema. "Sela anaweza kulichukuwa koti lako la mvua."



"Angalia soksi zangu. Ni ndogo sana," Nelima akasema.

"Kweli, ni ndogo," Mama alijibu. "Sela anaweza kuzichukuwa soksi zako."





"Angalia viatu vyangu. Ni vidogo mno," Nelima alisema.

"Ni kweli," Mama akajibu. "Sela anaweza kuvichukuwa viatu vyako."



"Sasa umepata nguo nyingi, sana," Nelima akamwambia Sela.

"La! Hasha!" Sela akajibu. "Hizi nguo zote ni kubwa sana kwangu!"

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way: Media Matters Author - Media Matters

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Sandy Lightly

Language - Kiswahili


Level - First sentences © African Reading Matters 2003

Creative Commons: Attribution-Non Commercial 3.0

Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)

Original source [www.read.org.za](http://www.read.org.za)





**READ**